MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 8 TOLEO 32

MACHI 25 , 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

HUU NI WAZIMU!

KUEZEKA KWA MA-KUTI MAHOTELI!



Benjamin. G. Mwalukasa



Mabaki ya hoteli ya kitalii ya Paradise Holiday

Na. Fred Katunzi

Kwa mara nyingine tena janga la kizembe na lisilo na sababu limetokea. Hoteli zilizojengwa kwa mamilioni (kama siyo bilioni) ya shilingi zimeteketea kama mabua shambani huku watu wakionekana kusikitishwa na matukio hayo ambayo yaliweka hatarani maisha ya watu kadha wa kadha.

Moto uliotekeketeza hoteli hizo za kitalii za Paradise Holiday na Oceanic Bay Resort huko Bagamoyo mkowa wa Pwani unakadiriwa kusababisha hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 13 kwani umetekeza kila kitu katika hoteli hizo na kuacha majivu na makaa.



Mkurugenzi wa Paradise Holiday Bw. Abdulai Nur Gulad aliyezungumza na gazeti la Mwananchi baada ya tukio alinukuliwa kusema "Nimeelezwa na wafanyakazi wangu kuwa moto ulianzia jikoni (na) ulisababishwa na hitilafu ya umeme na baadaye kusambaa kwenye majiko ya gesi na baadaye kushika makuti"

Huu ni upuuzi!

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI — MADINI YATATUOKOA?

Ushahidi unazidi kutiririka kuwa Tanzania kweli imejaliwa madini ya kila aina. Madini ambayo kwa watu wachache yamekuwa ni baraka lakini kwa taifa yamekuwa ni baraka kwa watu wachache!

Tunapoandaa sera mpya ya madini pamoja na sheria mpya katika kutekeleza mapendekezo ya wadau mbalimbali hatuna budi kujiuliza kama tuna uwezo na nia ya kutumia hazina hii tuliyojaliwa na Mwenyezi Mkuu kutupa maisha ya afueni.

Hata hivyo kwa kadiri tunavyotenda nina hofu kuwa yawezekana Mungu alikosoea kuipa nchi yetu hii utajiri wote huu kwani licha ya utajiri tulionao bado tumebakia kuwa maskini tukiendelea kuomba omba kama watu wasio na kitu.

Sijui itatokea lini tutambua kuwa hatuitaji mafuta kwenye ardhi yetu kuanza kuona sisi ni matajiri. Ukweli ni kuwa utajiri tayari tunao. Ni madini!

Ndani ya Toleo Hili

Kuezeka kwa makuti	1, 2
Hoja ya Mwanakijiji	1
Kuezeka kwa makuti	2
Mchungaji Mchokozi	3
DaJessy: Naunga mkono	3
Maoni ya Mtandao	4
Picha na Katuni	4

KUEZEKA HOTELI KWA MAKUTI

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo aliyefika eneo la tukio alinukuliwa kusema "Ujenzi huu ni hatari sana kwani moto ukishika kidogo, unaweza kusambaa katika maeno mengi kwa muda mfupi, ni vema sasa wamiliki wa hoteli wilayani hapa wakalitambua hili na kubadilisha aina ya uezekaji"

Inakadiriwa wafanyakazi kati ya 300 na 400 kati ya hoteli hizo mbili watakuwa wamepoteza chanzo chao cha kwanza cha kipato na wafanyakazi wengine wa sekta zilizokuwa zinategemea hoteli hizo nao bila ya shaka nao wataathirika. Hatuna budi kushukuru kuwa hakuna mtu aliyepoteza maisha yake katika matukio yote mawili.

Hata hivyo tunajikuta tukilaani ujenzi wa hoteli za namna hii kwa sababu ni wazi kuwa kuna watu ambao hawana kumbukumbu wala kujifunza kutokana na matukio ya nyuma. Ajali hizi mbili ni miongoni mwa ajali ambazo zinaweza kuepukika na kwa hakika msingi wake ni uzembe, tamaa ya fedha, kutokuwajibika na kwa hakika kukosa watu thabiti wenye kufanya maamuzi yenye manufaa huko mbeleni.

Mwaka 2007 hoteli ya Seacliff iliyoko nje ya Jiji la Dar iliteketea kwa karibu asilimia 75 na kusababisha hasara kubwa kwa hoteli hiyo, kuhatarisha maisha ya wafanyakazi na wageni na kuweka maisha ya waokoaji hatarini vile vile. Hoteli hizi zote tatu zimejengwa kwa kile kinachoitwa "kiutamaduni".

Tunadiriki kusema kuwa matumizi ya makuti katika majengo ya kisasa namna hii na ya kitalii ambayo yanaingiza mamilioni ya shilingi (kama siyo dola) ni upuuzi wa hali ya juu ni maandalizi ya majanga na kwa hakika jambo ambalo linastahili kukomeshwa mara moja.

Hakuna sababu yoyote ya msingi ya kwanini majengo haya yaezekwe makuti wakati kuna mabati na vigae vya kila aina ambavyo vingeweza kabisa kutumika kuezekea. Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa ni kufanya hoteli hizo ziwe za kitalii kweli kwa kuonesha "uafrika" au kuwa na ladha ya kiafrika. Hoteli hizi bila ya shaka vyumba vyake ni vina magodoro na si mikeka, na vitanda vyake ni vya kisasa siyo vya "telemka ni kukaze" na majiko yake ya kisasa siyo ya kupulizia kuni zimeshindwa kuona umuhimu wa kufanya ya kisasa mapaa yake!

Tunaamini kuwa kama kuna watalii wanataka kuona jinsi nyumba za makuti zilivyo, ni bora hoteli hizo ziandae vibasi vya kutembelea "uswahilini" ili watalii wajionee



na kwa kufanya hivyo kugawiana "utajiri" na sehemu zinazozunguka maeneo hayo. Njia nyingine ni pamoja na kuwapeleka kwenye maeneo ya sanaa au vijiji vya mfano. Kama watalii wanapenda kuona mazingira ya Watanzania katika utamaduni wao basi Wizara ya Utamaduni ifikiri jinsi ya kufanikisha hilo pasipo kuweka maisha ya watu na mali zao hatarini.

Tunapendekeza hatua zifuatazo:

a. Ujenzi mpya wa mahoteli haya uzingatie kanuni za ujenzi salama ambapo makuti na nyasi hazitatumika kuezekea. Katika hili kusiwe na na udhuru wowote. Hakuna hoteli inayohitaji kwa sababu yoyote ile kuezeka majengo yake kwa nyasi. Vinginevyo tufikie mahali katika kujivunia utamaduni tuezeke hospitali zetu kwa nyasi pia! Hivyo hoteli hizi zisiruhisiwe kabisa kuezeka kwa nyasi ya aina yoyote.

b. Mahoteli mengine ya kitalii nchini ambayo yana nyasi yapewa angalau muda wa miaka miwili kuezua nyasi zao na kutafuta mabati au vigae na kuondokana na nyasi hizi na mazingira haya ambayo ni ya hatari kwa watu na mali. Kama kuna mtu anaona raha ya kuishi kwenye nyumba za nyasi na kuwa ni fahari ya aina fulani mtu huyo aruhusiwe kubadilisha nyumba yake kuwa ya nyasi au kujenga nyuma ya nyasi lakini hilo lisiwepo kwenye majengo ya hadhara ya watu (public accommodation facilities).

Hilo linahusisha taasisi za shule, vyuo, na majengo ambayo watu wengi hukutana kwa sababu mbalimbali kwani ni majanga yanayosubiri kutokea.

c. Itungwe sheria ambayo itakataza makampuni ya bima kuweka bima kwenye majengo ya kibiashara yanayochukua watu wengi kwa wakati mmoja huku yakiwe yameezekwa kwa makuti, yasiyo na vifaa vya kuzimia moto au milango ya kutosha na ya kisasa ya wakati wa dharura. Tunakumbuka kuwa katika moto ule uliotokea Sea Cliff (Pichani kushoto) mmoja wa mabosi wa pale alizungumza pasipo na wasiwasi kuwa "tunayo bima".

Hofu yetu hapa ni kuwa majengo ya namna hii yanaweza kuwa mtaji wa baadhi ya watu kujijenga upya baada ya muda kwani bima italipa janga linapotokea. Tunatumaini hilo halijatokea katika majanga haya matatu ambapo bila ya shaka kiasi kikubwa cha fedha kitalipwa na yawezekana wajanja wakaanzisha moto kwa makusudi (arson) ili hatimaye waweze kupata zile fedha za kujenga upya mahoteli yao!

Ndiyo maana tunashuku mapema kauli zinazotolewa bila hata uchunguzi wa kitaalamu wa vyanzo vya moto kuwa moto ulianzia jikoni, ukashika mitungi ya gesi na kushika paa "lililoezekwa kwa makuti". Na ya kuwa kwa vile hoteli zenyewe ziko karibu na bahari upepo mkali bila ya shaka utarusha cheche kila kona. Je ikijakutokea cheche hizo zifikie kwenye maeneo ya makazi ya watu kutakuwaje?

d. Mwisho, tunashangazwa na kusikitishwa na kukosekana kwa magari ya kuzima moto katika mji mkongwe kama wa Bagamoyo. Zaidi ya yote, tunashangazwa na kukosekana kwa mipango ya haraka ya kuhakikisha kuwa kuna vyanzo vizuri vya maji katika maeneo haya hasa kutokana na umuhimu wake. Mji wa Bagamoyo ni mji mkongwe na unahistoria ndefu, hivyo bila mipango ya kisasa ya kuulinda mji huo (kama ilivyo miji mingine) ni wazii kuwa majanga kama haya yataendelea kutokea.

Nl lazima iwepo sera inayoeleweka ambapo kila Wilaya nchini iwe angalau na gari moja la kuzimia moto na kuwa na kikosi cha uokoaji (kiwe cha kujitokea au cha kuajiriwa).

Tunaamini pasipo kujiandaa kwa ma-

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

MAKUTI!

janga siku moja taifa letu litakuja kulipa gharama kubwa na wote kama kawaida tutakuwa wa kwanza kulia na kuanza kusema ni "mapenzi ya Mungu". Wakati umefika mapenzi ya wanadamu lazima yaanze kuinuliwa ili pale tutakapoamua kumwachia Mungu basi tujue ya kuwa kama binadamu tumefanya yote tuwezayo kujilinda.

Uzembe huu uliotokea Bagamoyo tunatoa wito ukomeshwe mapema kabla hatujashuhudia mambo kama haya. Tunapofikiria hilo hatuna budi kujiuliza kama kuishi katika nyumba za nyasi na majani ndiyo utanzania wenyewe? Je kuna sera yoyote ya nyumba na makazi ambayo inakusudia kumuondoa Mtanzania kutoka katika nyumba za nyasi, makuti na udongo na kumfanya aishi kwenye nyumba bora na ya kisasa? Au nyumba za namna hiyo ni za wale waliofanikiwa kimaisha tu na si haki ya kila Mtanzania?

Tupange kwa makusudi kuwa kizazi chetu kiweze kuona nyumba za makuti na nyasi zinabakia sehemu za makumbusho.

MCHUNGAJI MCHOKOZI

Rev. Kishoka



Leo hii tunapingana na kubishana kuhusu Rostam, Lowassa, Lukaza, Chenge, Karamagi, Jeetu na wengine wengi ambao wamehujumu nchi yetu. Lakini mkondo wa haki na sheria ni butu, vyombo vya dola vinaogopa wahujumu hawa maarufu kama mafisadi, wanasiasa na wakubwa wa mashirika wanashirikiana na hawa mafisadi kuhujumu nchi na hakuna anayediriki kuona soni na kuwajibika au kukaripia uhujumu na ufisadi.

Sasa kama tuliowapa dhamana ya kutulinda na kutoa haki wanashindwa kazi zao na kila tukichagua watu wapya, tunakuta mizizi iliyokomaa ya hujuma na ufisadi imetambaa kama gonjwa la Ukimwi au Satarani, basi kwa nini tusichukue hatua mikononi?

Leo mwizi wa kuku, redio au tairi la gari hupewa mkong'oto mkali na huswekwa jela akibahatika kufika huko akiwa hai, lakini wanaotuhujumu kwa mabilioni, ndio kwanza wanakaribishwa kukata tepe, wanapokelewa kwa maandamano na bado wanaendelea kupelelezwa kisa eti ushahidi hautoshi au wapepelezi na waendesha mashitaka wanasubiri ridhaa ya Rais kufungua mashitaka?

Nasema bila woga, pamoja na kuwa ni kinyume cha haiba yangu, wakati umefika, tujichukulie hatua mikononi, tuanze kuwapiga mawe na kuwachapa kila aliyeshindwa kazi na kutuingiza katika umasikini kwa kutuhujumu.

Sijali awe Rostam, Mkapa, Chenge, Karamagi, Lowassa, Lukaza, Vithlani, Patel au Mattaka, kama kuna kiongozi au mtendaji ambaye ametuingizia hasara ambayo ni kutokana na uhujumu, sherti tumchape viboko akiwa ma ta ko wazi hadharani, kisha tumtembeze nchi nzima akiwa uchi kama tunakimbiza Mwenge au wale vikojozi mtaani azomewe, achapwe mijeledi na hata tumpige mawe.

Labda hapo tutakapoamka na kujichukulia sheria mkononi, Wanasiasa wetu watakuwa na adabu na kujifunza kuchapa kazi na kuwa waadilifu na wanyenyekevu!

DADA Jessy: MABINTI HAWA NI WA KUUNGWA MKONO!

Na. Jessica L. Fundi

Ninaona fahari wiki hii tena fahari ya kunifanya nipige vigelegele. Fahari ya kuona mabinti zetu wameweza kusimama kupinga ufisadi wa ngono na unyanyasaji wa kijinsia. Wiki hii wanafunzi wa kike katika shule ya sekondari ya Lupanga wilayani Morogoro waligoma baada ya kuwatuhumu walimu wao watano wa kiume kuwa wamekuwa wakiwataka kimapenzi na kuendeleza vitendo vya ngono na wanafunzi.

Tuhuma hizi ni nzito dhidi ya mtu yeyote lakini inapotolewa dhidi ya walimu jibu la kwanza ni kuegemea upande wa tahadhari mara moja na kuwa upande wa watoto hawa. Kilichonishangaza ni kuwa hadi hivi sasa hakuna utaratibu unaokubalika (standard operating procedure) wa kushughulikia tuhuma za unyanyasaji wa ngono mashuleni. Kama taratibu hizo zipo basi hazijulikani na kama zinajulikana na ndizo zilizofuatwa huko Morogoro tuna kila sababu ya kuwa na hasira.

Mabindi hawa wamewatuhumu watu walio na madaraka juu yao na walimu wao. Kutokana na uzito wa tuhuma



hizo binafsi nilitarajia walimu hao wangesimamishwa mara moja (huku wakilipwa) ili kupisha uchunguzi huru. Kilichonishangaza ni Mkuu wa Shule hiyo kuitisha kura ya wanafunzi kuona ni nani atawataja walimu hao ili baadaye "bodi" ifikirie hatua za kufanya.

Hadi kwenda Mkuu wa Wilaya (Pichani) kuzungumza na wanafunzi hawa ni kuongeza utisho kwa watoto hawa ili wasiweze kuzungumza tena matukio ya namna hii. Ni jukumu letu kama jamii kuhakikisha kuwa tunatengeneza mazingira bora ya mafunzo na watoto hawa wasijikute wanaadhibiwa. Ni wazi kuwa haiwezekani katika shule hiyo walimu hao kuendelea kufundisha katika mazingira ya shuku. Ni vizuri kuwapa moyo mabinti zetu na hata watoto wengine kuwa na ujasiri wa kusema na kuambia vyombo husika juu ya vitendo vya namna hii. NI jukumu la walimu wa kuu na viongozi wahusika kuchukua hatua mara moja kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakuwa salama na kutowaacha mikononi mwa walimu ambao ni mafisadi wa ngono. Ipo mifano mingi katika jamii ambapo walimu wamekuwa wakifanya vitendo hivi bila ya kujali matokeo yake.

Binafsi nawapigia makofi mabinti hawa kwa kitendo chao cha kijasiri. Tuhakikishe kuwa sheria ya Makosa ya Kujamiiana inafuatwa na watu wote na hasa wale walio na amri juu ya watoto wetu!

Niandikie: dajessy@klhnews.com

Soma bure

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Wiki



Mkazi wa Mtoni Kijicha akijaribu kuzima moto kwa kikombe. Je ndiyo juhudi zetu zilivyo dhidi ya ufisadi?


JIUNGE NA WANAKIJIJI WENZAKO!

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia sisi!

KATUNI ZA WIKI





KUTOKA KWENYE MTANDAO

Sisi Tunawatu wanaolala hoi, wanaosubiri Masiha ashuke kuwakomboa, Sisi tunamawazo lakini hatuwezi kuingia barabarani kuwaambia sasa inatosha waondoke, kwani nikifanya hivyo mwanangu hatasoma tena, nitapigwa risasi na kikosi cha Fanya Fujo Uone, sisi hatuwezi kuwaondoa kwenye karatasi, kwani tunaogopa kuwachagua wengine tutauza nchi, tumeambiwa tutakaribisha Vita.

Nia Tunayo mzee, sababu Tunayo, lakini Uwezo wetu ni mdogo sana kama unavyotuona kwenye picha—**Mbogela**

Mrema si kiongozi makini na ni myumbishaji mkubwa wa upinzani...yuko kwenye upinzani kwa maslahi ya CCM.—**Ndesamburo**

Awamu hii ya JMK hata sijaielewa maana inaonekana ni Kama vile "Bora Liende" ili mradi ni kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya.
Kila nikitembelea maeneo haya tunayoishi, Mwananyamala, tandika, kigogo, Survey, Tandale, manzese nilikuwa nahofia siku Moto utakapotokea na hii ndio hali halisi tunavyoiona sasa.—**Anon**

Jamani hivi sisi tumelaaniwa yaani kweli gari la zima moto litoke dar kweli mpaka bagamoyo,hawa wabunge ,wakuu wa wilaya na wakurugenzi hata mwenye hotel wanafikiria nini mi naona akipewa kibano mmoja hadi afe ndio watawajibika.– **Anon**

Mfano lazima uwe na pampu za maji karibu na bwawa la kuogelea au ambazo zina mipira ya kuweza kufika baharini.Pia hayo makuti yana dawa ambazo zinawekwa ili zisishike moto au zisiungue haraka.

Kama umewekeza mabilioni ya shilingi na huchukui tahadhari hizo basi mimi sikuelewi. **Ray**

Soma Bure
hoja zenye nguvu

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha, maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: **Mhariri@klhnews.com**

Tovuti: **http://www.mwanakijiji.com**

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*